



EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

MAOMBI YA TAARIFA YA KUONYESHA NIA KWA AJILI YA UTOAJI HUDUMA ZA UTHAMINI KWA AJILI YA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP) – KUMBUKUMBU NA: 10006677

TOTAL East Africa Midstream B.V (Kampuni) Tanzania, kampuni ya Mafuta na Gesi, inaalka makapuni yenye uzoefu na sifa kuonyesha nia ya kutoa huduma za uthamini katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini la kusafirisha Mafuta linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha Mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania. Eneo la bomba katika upande wa Tanzania litakatiza Mikoa nane (8), ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga. Bomba litapita katika Mamlaka za Halmashauri za Wilaya 27 na Vijiji 231.

MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:

Mradi unahitaji mkuza wa ardhi kwa ajili ya bomba na miundo mbinu ya juu ya ardhi na kwa ajili ya ujenzi na uendeshaji wa Bomba la Mafuta Ghafi. Utwaaji wa ardhi unalazimu malipo ya fidia chini ya mfumo wa sheria za Tanzania na uzingatiaji wa Mipango Kazi ya Uhamishaji wa Watu na Makazi ya Mradi na Viwango vya Uwezeshaji wa Fedha vya Kimataifa (IFS). Vilevile, Mradi utagharamiwa na wawekezaji hivyo, utoaaji wa ardhi mbadala kwa ajili ya kilimo na makazi kwa Waguswa wa Mradi itahitajika.

Kampuni inahitaji huduma za kampuni za Kitanzania zenye sifa, uzoefu na zinazoweza kutoa Wathamini wa Kitanzania waliosajiliwa na kukidhi vigezo vya kutoa huduma za viwango vinavyohitajika kusaidai Mradi.

Mawanda ya kazi ni pamoja na:

- Kuwaelewesha Waguswa wa Mradi wa EACOP juu ya stahiki zao chini ya sheria ya Tanzania na viwango vya Kimataifa vya Uwezeshaji wa Kifedha;
- Kuwasaidia Waguswa wa Mradi na Mradi katika kusaini mikataba ya fidia;
- Ubainishaji, ukaguzi, utafiti na uthamini Ubainishaji, ukaguzi, utafiti na uthamini kwa ajili ya manunuzi ya ardhi mbadala ya kilimo au makazi.

Mawanda ya kazi yatahitaji uwepo binafsi wa mfanyakazi wa MKANDARASI atakaye chaguliwa katika eneo husika na pia kuwa na muingiliano wa moja kwa moja na kaya chini ya usimamizi na muongozo wa mfanyakazi wa KAMPUNI.

VIGEZO MUHIMU:

Makampuni yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa usajili wa Ofisi ya Uthamini katika Bodi ya Usajili wa Wathamini.
- Uthibitisho wa usajili wa Wathamini wa Kampuni ya Uthamini katika Bodi ya Usajili wa Wathamini.
- Uthibitisho wa usajili katika Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) na Cheti cha Ithibati ya Malipo ya Kodi cha mwaka wa hivi karibuni.
- Maelezo kwa ufupi ya uzoefu wa kutoa huduma za uthamini chini ya sheria za Tanzania na Viwango vya Kimataifa vya Uwezeshaji wa Kifedha katika miradi mikubwa nchini Tanzania na katika jamii zilizo maeneo ya vijijini.
- Wasimamizi wanaopendekezwa kufanya kazi na wahusika katika timu ya Mradi pamoja na uzoefu wao katika kutoa huduma kama hizi.
- **Usajili katika Kanzi Data ya Watoto Huduma wa Ndani ya EWURA (LSSP) katika kipindi cha kuwasilisha majibu ya nia kwa ombi hili unahimizwa.**

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: mihye.allaire@external.total.com (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa 11:00 jioni Majira ya Afrika Mashariki, tarehe Friday 16th Aprili 2021.

Muhimu: Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapatia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).